# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani,
Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA MAWASILIANO, ARDHI NA NISHATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** kila sifa njema zinamstahikia Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehma, kwa kutujaalia Uzima na Afya njema ambavyo vimetuwezesha kukutana tena katika Baraza hili la Kumi kwa lengo la kuendelea kuwatumikia wananchi wetu. Vile vile, nachukuwa fursa hii kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Baraza kwa kuliongoza Baraza hili Tukufu kwa umahiri mkubwa na ninaamini kwamba mtaendelea kuliongoza Baraza hili kwa uadilifu wa hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, napenda kuchukuwa fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuiongoza nchi hii kwa uadilifu, hali inayopelekea kupatikana kwa maendeleo pamoja na kuendelea kudumu kwa amani na utulivu katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia inampongeza Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa shughuli za Serikali yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, sina budi kumshukuru Waziri wa Maji, Nishati na Madini Mhe. Shaib Hassan Kaduara na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Zawadi Amour Nassour kwa umahiri mkubwa wa uongozi wao, Pia, tunawapongeza watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu bila ya kuwasahau watendaji wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mashirikiano waliyotupatia wakati wa kupitia makadirio ya Bajeti ya Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, nachukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii kwa umoja wao na kazi nzuri waliyoifanya kiasi cha kunirahisishia kazi ya kuongoza vikao kuwa nyepesi zaidi, kwa hakika ni Wajumbe mahiri, wameweza kuijadili ipasavyo na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha zinazoidhinishwa kwa Wizara hii zinatumiwa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima ya hali ya juu kabisa napenda kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Yahya Rashid Abdulla | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Aza Januar Joseph | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Fatma Ramadhan Mohammed | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Simai Mohamed Said | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Hudhayma Mbarak Tahir | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| *6.* | Mhe. Mwanajuma Kassim Makame | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Ameir Abdalla Ameir | Mjumbe |
| *8.* | Mhe. Hassan Hamad Omar | Mjumbe |
| *9.* | Mhe. Haji Ussi Haji | Mjumbe |
| *10.* | Ndg. Himid Haji Choko | Katibu |
| *11.* | Ndg. Saad Othman Saad | Katibu |
| *12.* | Ndg. Salma Muhsin Haji | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,** Mapato ya wizara hii kiujumla na kiwastani yanaridhisha ambapo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi **15,285,400,000** na hadi kufikia kipindi cha Julai – Machi 2023/2024 makadirio ya makusanyo ni **11,425,498,500** ambapo wizara imekusanya jumla ya shilingi **11,713,375,451** sawa na asilimia 103.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Kwa upande wa mapato kwa Taasisi zilizochini ya wizara hii, kuna baadhi ya taasisi makusanyo yake hayaridhishi na taasisi nyengine zinaonekana kukusanya vizuri zaidi. Hadi kufikia Julai – Machi 2024, ZURA imefanikiwa kukusanya jumla ya Asilimia 107 ambapo imevuka kiwango cha makadirio ya makusanyo na Shirika la Umeme (ZECO) ni Asilimia 92 na Kwa upande wa ZAWA imekusanya Asilimia 44. Kamati inazisisitiza taasisi hizo kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato hasa kwa Mamlaka ya Maji (ZAWA) kwa vile tunatarajia usambazaji na uunganishaji wa maji utafikia hatua nzuri kwa kupata maji majumbani mwetu hali itakayoongeza makusanyo maradufu kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini katika kusimamia na kutekeleza Bajeti ya fungu lake la NO3 ina jumla ya Programu Kuu tatu *(3)* ambazo ni Programu PNO301 – Usimamizi wa Huduma za Maji, Programu PNO302 – Usimamizi wa Huduma za Nishati na Madini na Programu PNO303 – Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini. Kamati imeyapitia mafungu hayo kwa umakini na inashauri kuwe na usimamizi mzuri wa utendaji ili maendeleo ya sekta zilizomo katika wizara hii ziwe mwanga na mfano kwa maendeleo ya jamii hii.

## PROGRAMU YA USIMAMIZI WA HUDUMA ZA MAJI

**Mheshimiwa Spika,** Hali ya Uzalishaji wa maji kwa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba hadi kufikia Machi 2024, mahitaji ya maji yamefikia lita **275,980,481** na uzalishaji ni lita **191,959,675** kwa siku sawa na Asilimia 70 ya uzalishaji na kuna upungufu wa maji wa lita **84,020,806** sawa na asilimia 30 za mahitaji. Kamati haijaridhishwa na uzalishaji wa maji ambapo kwa mwaka jana hali ya uzalishaji ilikuwa ni Asilimia 67 hali inayoonesha kuna ongezeko la Asilimia 3 tu la uzalishaji kwa kipindi cha Julai – Machi, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha *2024/2025,* Wizara ya Maji, Nishati na Madini pamoja na Taasisi zake imelenga zaidi katika kukuza na kusimamia vyema sekta ya maji na kuhakikisha huduma ya maji safi na salama inapatikana kila sehemu tena kwa uhakika na kuwa endelevu kwa wananchi wote wa Zanzibar, hii inatokana na kujipanga katika kuendeleza miradi mbali mbali ya maji ili kuhakikisha maji yanawafikia wananchi wakati wote. Kamati inaisisitiza Serikali kwamba shughuli za usambazaji na

uunganishaji wa huduma ya maji katika nyumba za wananchi (House Connection) uwe wenye tija na ukamilike kwa haraka ili wananchi wafaidike na azma ya Mheshimiwa Rais wetu Mpendwa ya kumtua mama ndoo kichwani. Aidha, Kamati pia inaishauri Serikali kuwa miundombinu ya mita inayoekwa kwenye Shehia za Mitaa yetu iwe ni rafiki kwa matumizi na yenye kulinda mazingira na mandhari mazuri ya maeneo yetu pamoja na kuimarisha ustawi wa miundombinu mingine hasa Barabara za ndani.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini bado kuna tatizo la ukosefu wa maji katika shehia zetu hususan kwa maeneo ya ukanda wa pwani ambapo baadhi ya wananchi wanatumia maji ya chumvi kwa matumizi ya kawaida na maji safi wananunua kwa ajili ya matumizi ya kunywa tu. Kamati inazishauri taasisi zote za Serikali zenye mnasaba na upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kushirikiana kwa pamoja ili huduma hii iwafikie wananchi wote, vile vile tunawaomba wananchi wawe na moyo wa uzalendo wa kutunza miundombinu na vyanzo vya maji kwa manufaa ya kizazi chetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza wizara kwa kukiimarisha chuo cha kati cha Maji kilichosajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) ambacho uongozi wake uko chini ya wizara hii kupitia ZAWA. Kamati inaunga mkono Serikali kupitia ZAWA kuwa upo umuhimu wa kuendelea kuwepo kwa chuo hicho chini ya wizara hii, hasa kwa vile wao ndio wanaofungamana na utaaalamu pamoja na uzoefu mahsusi wa utoaji wa huduma ya maji. Aidha, uzoefu wa Kamati unaonesha kwamba takriban vyuo vyote duniani vinavyoendeshwa chini ya

Taasisi za huduma husika vinakuwa bora na vyenye mafanikio zaidi na huwezesha kutatua changamoto zinazowakabili za kiutendaji kwa muda mfupi.

## PROGRAMU YA USIMAMIZI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MADINI

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Hotuba ya Mheshimiwa wa Maji, Madini na Nishati ya mwaka wa fedha 2024/2025 inaeleza**, h**ali ya Uzalishaji wa umeme yamekuwa kwa wastani wa Megawati 21.3 kati ya mwaka 2021 hadi 2024 ambapo waya unaosafirisha umeme uko ukingoni kiuwezo wa matumizi ya waya wa megawati100 umefikia megawati 90.8 na kwa waya wa megawati 45 yamefikia megawati 30 ambayo ni sawa na asilimia 83 ya uwezo wa waya huo kwa upande wa Unguja. Aidha, kwa upande wa Pemba mahitaji ya juu ya umeme ni megawati 13.50 sawa na Asilimia 67.5 ya uwezo wa waya unaotumika wa megawati 20. Hivyo, Kamati inashauri katika kuendeleza sekta ya umeme, Serikali kupitia Shirika la Umeme (ZECO) iwahamasishe na iwaruhusu wawekezaji binafsi kuwekeza katika sekta ya umeme kwenye maeneo ya miradi yao mbali mbali mfano Mahotelini ili kupunguza tatizo la upatikanaji wa umeme mdogo katika nchi yetu ambao wanaweza kuutumia na umeme mwengine wa ziada wakawauzia ZECO.

**Mheshimiwa Spika,** Umeme ni sekta nyeti na chachu ya maendeleo inayounganisha na kurahisisha hudumu nyengine mbali mbali za wananchi kiuchumi na kijamii, kuwepo kwa uhafifu, umeme mdogo na kukatika kwa huduma hii kunasababisha kufiyaya kwa harakati za Serikali na wananchi

kiujumla. Kamati inalishauri Shirika la Umeme – Zanzibar (ZECO) kuilinda miundombinu ya umeme kwa kuyabaini na kuyaekea alama maeneo yaliyochini na yaliyoizunguka miundombinu hiyo ambayo ni hatarishi kiafya hasa yale waliyoyavamia wananchi kwa ujenzi na shughuli nyengine za Kijamii na Uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** Kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa wizara hii imeeleza katika kipindi cha Julai hadi Machi 2024, Shirika la Umeme limebadilisha jumla ya nguzo mbovu 1,661 ambapo kwa upande wa Unguja 1,344 na Pemba ni nguzo 317. Kamati imebaini kwa mwaka Serikali inatumia gharama kubwa za ubadilishaji wa nguzo mbovu za umeme hali inayopelekea kupoteza muda katika shughuli za ubadilishaji, nguvukazi (watumishi) na kukosa huduma katika kipindi cha matengenezo jambo ambalo haliridhishi kiutendaji na kwa wapokeaji wa huduma. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kujikita kwenye utaratibu wa kuweka nguzo za zege kama ilivyokuwa zamani, pia ziwe na rangi maalum itakayopendekezwa na Serikali kwa ajili ya kupendezesha mji wetu (beautification) badala ya nguzo tulizonazo miti. Pia, Serikali ihakikishe katika uwekaji wa nguzo mpya za zege uzingatie ubora na viwango vya kitaalamu vya uwekaji wa msingi wa nguzo hizo (Installation) ili kuongeza uimara wa kudumu kwa nguzo hizo kwa zaidi ya miaka Sabiini (70) inayokadiriwa.

**Mheshimiwa Spika,** Athari ya uhaba wa mafuta katika nchi yetu hupelekea kudumaza shughuli za kimaendeleo na kiuchumi. Kamati inaishauri ZURA kuweza kuzibaini changamoto za viashiria vya upungufu wa Mafuta kabla yakutokea, na pindi changamoto za viashiria hivyo vikitokea Serikali kutoa

taarifa za awali kwa wananchi wote kupitia vyombo mbali mbali kwa lengo la kuwafikia wanajamii wa nchi nzima.

**PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA MIPANGO YA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini changamoto ya wataalamu katika fani mbalimbali zikiwemo Wahandisi, Mafundi pamoja na wataalamu wa Mafuta. Kamati inaishauri Serikali kupitia taasisi zake ZAWA, ZURA na ZECO kuongeza kasi ya kuwajengea uwezo wafanyakazi wao kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mafunzo ya muda mfupi ili kuweza kukidhi mabadiliko ya utoaji wa huduma hizo Kitaifa na Kimataifa hasa kwa vile taasisi zilizomo ndani ya wizara hii ni muhimu sana kwa wananchi ambapo wanahusika moja kwa moja katika kuendesha shughuli za maendeleo za kila siku za kijamii na Uchumi wa nchi. Aidha, utaalamu huo uendane na udhibiti wa changamoto za kiushindani duniani ambazo huibuka zaidi kupitia mikutano na Makongamano mbalimbali ya Wadau ya Kikanda yanayohusu ubora wa huduma na viwango vya bidhaa hususan Mafuta.

*HITIMISHO*

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia hotuba hii, nachukuwa fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu kwa niaba ya Kamati pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa wakati wote wa uwasilishaji wa maoni yetu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia Kamati imeona kwamba majukumu mengi ya taasisi za Serikali hayawezi kufanyika ipasavyo kutokana na kutoingiziwa fedha kwa wakati na kwa mujibu wa kilichopangwa katika bajeti zao. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuingiza fedha kwa wakati na kwa mujibu wa zilivyopangwa ili ufanisi wa kiutendaji uweze kupatikana kwa maendeleo ya wananchi na nchi yetu kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waichangie Bajeti hii na hatimae waidhinishe makadirio ya mapato na makadirio ya matumizi kwa Wizara ya Maji, Nishati na Madini kama yalivyopangwa kukusanywa na kutumiwa kwa mwaka wa fedha *2024/2025*.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati yangu ***Naomba Kuunga Mkono Hoja.***

Ahsante,



……………….……………..

**Yahya Rashid Abdulla**
Mwenyekiti,
Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**